# ATOAYE KWA MOYO MKUNJUFU

## (Darasa la Tisa)




Mch. Denis & Devis Julius

# ATOAYE KWA MOYO MKUNJUFU.

## Utangulizi.

Mafundisho maalumu kwa Watoto umri (0-12).

Mafanikio ya mtoto, kiroho na kimwili hayaji peke yake pale tu, anapojifunza njia za wokovu, na kuwaheshimu wazazi, au kuwa na tabia njema. Lakini yanachangiwa pia kwa sehemu kubwa na UTOAJI.

Utoaji si fundisho tu, linalowahusu watu wazima, bali ni fundisho, linalopaswa kufundishwa kwa Watoto angali wakiwa wadogo kabisa.

Mungu wetu, leo hii tunamtumikia, tunamwabudu, tunampenda, kwasababu ya karama yake kubwa aliyoidhihirisha kwetu ya kutoa. Alitoa dunia yake bure, sisi tuweze kuishi humo, alitoa na mimea yake, maji, hewa, upepo, jua, mwezi, Wanyama bure, ili sisi tuweze kunufaika katika hivyo hapa duniani.

Lakini kubwa zaidi alimtoa mwanawe mpendwa, Yesu Kristo kama sadaka kwa kufa pale msalabani awe fidia ya dhambi zetu,. Na hata sasa bado Mungu anatoa Fadhili zake nyingi zisizohesabika, kwa wanaomwomba na hata wale wasio mwomba.

Na yeye anataka watu wake wawe wote na tabia hiyo kama yake.

Hivyo mtoto anapaswa afundishwe Kutoa, kama sehemu ya fundisho kuu la maisha yake, ili afanane na Mungu. Wakati mwingine watalaumiwa watu kuwa wabinafsi, kumbe chanzo ni misingi waliyokuzwa nayo tangu wakiwa wadogo.

> *Mithali 22:6 Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee*.

Hili ni darasa la Tisa (9), Ikiwa hujapata madarasa ya nyuma, basi mwisho wa chapisho hili, kuna mawasiliano, tumia namba hizo kuwasiliana nasi.

Mungu akubariki.

## **Moyo Mkunjufu.**

Kifungu Mama cha kusimamia, cha kumpa mtoto akikariri:

> *2Wakorintho 9:7 Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu.*

Mwl: Awali ya yote mtoto anapaswa afundishwe kuwa Kutoa si jambo la kulazimishwa, au amri, bali ni jambo la moyoni. Kwamba anapaswa aone Fahari kutoa, kama tu vile anavyoona Fahari kupokea. Mjengee fikra kuwa kutoa sio adhabu bali tendo la upendo lililobarikiwa na Mungu.

## **Ni nini napaswa kutoa?**

Mwl: Mfundishe mtoto kwamba kile alichonacho ndicho anachopaswa kutoa. Asitoe cha mwingine kama hajapewa ruhusu, asiibe kitu nyumbani na

Kwenda kukitoa, ili kutimiza agizo la utoaji. Kile alichonacho hata kama ni kidogo, anao wajibu wa kutoa.

Ukisimamia andiko hili,

> *2Wakorintho 8:12 Maana, kama nia ipo, hukubaliwa kwa kadiri ya alivyo navyo mtu, si kwa kadiri ya asivyo navyo.*

## **<u>Mfano wa vitolewavyo ni vipi?</u>**

"Pesa"

"Chakula"

"Mavazi"

"Vitu"

"Muda"

## **<u>Ni nani wa kumtolea:</u>**

<u>Mungu:</u>

Mfundishe mtoto wa kwanza wa kumtolea ni Mungu

Na tunamtolea kwa njia ipi? Kwa njia ya sadaka, mfundishe mtoto kila aendapo ibadani, ahakikishe anamtolea Mungu. Kwamba Mungu hapendezwi na

mtu anayekwenda nyumbani mwake mikono mitupu (Kumbukumbu 16:16), Na kwamba ni tunapomtolea tunaonyesha kitendo cha heshima kwake.

> *Mithali 3:9 Mheshimu Bwana kwa mali yako, Na kwa malimbuko ya mazao yako yote.*

<u>Maskini:</u>

Hawa ni watu wenye uhitaji sikuzote, wanaweza wakawa ni Watoto yatima, au fukara, ambao hawana chakula, mavazi, au malazi. Mungu ametuagiza kuwasaidia kwa vile tulivyo navyo.

> *Mithali 19:17 Amhurumiaye maskini humkopesha Bwana; Naye atamlipa kwa tendo lake jema.*

<u>Mwingine yoyote mwenye uhitaji:</u>

Huyu Si lazima awe, maskini, lakini anaweza kuwa rafiki au ndugu, au jirani pengine wamepungukiwa na hitaji mojawapo, na wewe unacho cha kumpa, yakupasa umpe, kama Yesu alivyoagiza.

*Mathayo 5:42 Akuombaye, mpe; naye atakaye kukopa kwako, usimpe kisogo*

## **Kanuni bora za utoaji:**

Usitarajie kulipwa:

Mwl: Mfundishe mtoto, kuwa asitoe kwa lengo la kurudishiwa mema kwa yule aliyempa zaidi sana awekeze kwa watu ambao hawawezi kumlipa kama Bwana Yesu alivyoelekeza katika Luka 14:12–14

*12 Akamwambia na yule aliyemwalika, Ufanyapo chakula cha mchana au cha jioni, usiwaite rafiki zako, wala ndugu zako, wala jamaa zako, wala jirani zako wenye mali; wao wasije wakakualika wewe ukapata malipo. 13*
*Bali ufanyapo karamu waite maskini, vilema, viwete, vipofu,*
*14 nawe utakuwa heri, kwa kuwa hao hawana cha kukulipa; kwa maana utalipwa katika ufufuo wa wenye haki.*

Usijionyeshe:

Mfundishe mtoto Kutoa kwa lengo la kusifiwa au kutazamwa na watu, kunaharibu utukufu na sifa ya sadaka hiyo, bali mfundishe kufanya wema wake kwa siri.

*Mathayo 6:2*

*2 Basi wewe utoapo sadaka, usipige panda*
*mbele yako, kama wanafiki wafanyavyo katika*
*masinagogi na njiani, ili watukuzwe na watu.*
*3 Amin, nawaambieni, Wamekwisha kupata*
*thawabu yao. Bali wewe utoapo sadaka, hata*
*mkono wako wa kushoto usijue ufanyalo mkono*
*wako wa kuume;*
*4 sadaka yako iwe kwa siri; na Baba yako*
*aonaye sirini atakujazi.*

## **Faida za kutoa:**

Unakubaliwa na Mungu:

Mwl: Mfundishe kuwa, Habili alikubaliwa na Mungu zaidi ya ndugu yake Kaini, kwasababu alimtolea Mungu sadaka iliyo bora, na ya kwanza. Kornelio alikubaliwa na Mungu kwasababu ya sadaka zake nyingi alizomtolea Mungu. (Matendo 10).

Hivyo na yeye anapokuwa mtoaji mwaminifu, atakubaliwa na Mungu mfano wa hao.

Unabarikiwa:

Wafundishe, kumtolea Mungu ni chanzo cha kubarikiwa zaidi, ikiwa atatoa pesa yake kama sadaka, inafanyika kuwa mbegu ambayo ataivuna baadaye kwa vingi, akiwapa watu vitu na yeye pia atapewa kwa kipimo cha kusukwa-sukwa na kujazilishwa.

> *Luka 6:38 Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwa-sukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa.*

## Wimbo:

Wafundishe Watoto pambio au wimbo wowote, wenye maudhui ya utoaji kwa Mungu,. Ukimfundisha mtoto kwa njia ya nyimbo fundisho hukaa ndani yake vizuri zaidi kuliko maneno tu.

## Igizo:

Igizo pia humrahisishia zaidi mtoto, kuliweka fundisho moyoni mwake muda mrefu.

Hivyo unaweza wachukua Watoto wawili au watatu, au zaidi.

Waweke kwenye makundi mawili,

Kundi la kwanza: Mmoja anaigiza kama mzazi anayempa mwanaye pesa ili akatoe sadaka kanisa.

Kisha mtoto anakwenda kanisani, na mara anakutana na mwenzake, anamshawishi waitumie ile sadaka kununua soda, huyu aliyepewa anakataa na kumwambia. Mungu hatatubariki, au kutupenda ikiwa tutaitumia sadaka kwa matumizi yetu wenyewe, hatatukubali. Kisha yule mwenzake anatubu anasema ni kweli, lazima Tubarikiwe na Mungu,na tukubaliwe na yeye kama Kornelio. hivyo twende tupeleke sadaka zetu kanisani.

Kisha andaa igizo lingine: Mmoja anajifanya anakula chakula njiani, labda keki kisha maskini anamfuata na kumwomba amemgee kidogo keki, kisha anakataa. Lakini anaenda mbele kidogo, anakumbuka lile andiko linalosema, wapeni watu vitu, nanyi mtapewa, kipimo cha kusukwa sukwa na kujazilishwa, ndivyo watu watakavyowapa kifuani mwenu.

Anarudi na kummegea yule maskini, sehemu ya keki yake, kisha anaondoka kwa furaha, akijua kuwa Mungu anakwenda kumbariki zaidi.

## Kuinenea Sadaka:

Ni vema kumfundisha pia mtoto kuinenea sadaka yake, anapoipeleka madhabahuni kwa Mungu.

Kila atoapo mfundishe kuisema sala hii ya baraka:

> ***Bwana Yesu sadaka yangu ninayoitoa ikawe mbegu ya baraka na mafanikio yangu ya kiroho na kimwili.***

## Zoezi la Nyumbani:

Usimwache mtoto, bila jukumu la wiki. Mwambie, pesa utakayopewa na wazazi shuleni kwa ajili ya chakula, hakikisha huitumii yote, tenga kidogo, leo shilingi kumi, kesho kumi, hivyo hivyo mpaka wiki inapoisha kisha ujapo kanisani, uitoe hapa madhahabuni.

Hilo litamjengea mtoto nidhamu ya kumtolea Mungu katika vile vyake mwenyewe, sio vile anavyopewa siku ya ibada na mzazi ili amtolee Mungu.

## Agizo kwa Wazazi

Watoto waseme mbele ya kanisa.

*Wazazi tujengeeni msingi wa kupenda kumtolea Mungu katika vile mnavyotugawia sisi kama vyetu, ili tubarikiwe*.

Wazazi wakisikia ombi la Watoto, fundisho litahama kutoka kwako Mwalimu, litaendelea kwa wazazi. Pia waaagize, si kila wakati wawape Watoto moja kwa moja sadaka, bali wawape vya kwao, kisha ndio watenge katika hivyo fungu la sadaka, wawakague siku ya Kwenda ibadani, kama wametenga fungu hilo.

Bwana akubariki.

**Mawasiliano:**

Kanisa la Nuru ya Upendo

+255693036618 \ +255789001312

Mch. Denis & Devis Magembe

info@wingulamashahidi.org

www.wingulamashahidi.org